**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA WAZIRI MKUU – TAMISEMI**

SHULE YA SEKONDARI KAGOMA

S.L.P 268,
MULEBA-KAGERA
TAREHE……………………………

NAMBA ZA SIMU
MKUU WA SHULE; 0762972449 Au 0686563233
MAKAMU MKUU WA SHULE (ADVANCE) 0777523527 au 0755220635
MAKAMU MKUU WA SHULE 0715160651 Au 0753160651
MZAZI/MLEZI WA …………………………………………………………………………………….. ( Jina la mwanafunzi)
S.L.P……………………………………………

**YAH: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI KAGOMA HALMASHAURI YA WILAYA MULEBA MKOA WA KAGERA MWAKA ……..**

Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na kidato cha tano katika shule ya sekondari Kagoma mwaka …….. Tahasusi………………………………

Shule ya sekondari Kagoma iko umbali wa kilomita tisa(9) Kaskazini mwa Mji wa MULEBA. Usafiri wa pikipiki kutoka MULEBA mjini unapatikana katika kituo cha Mabasi kwa TSH. 2000 hadi TSH. 3000. Na kwa usafiri wa magari yanayoelekea BUKOBA nauli ni TSH. 1000.

Muhula wa masomo utaanza tarehe ……….Hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni tarehe …………. Mwisho wa kuripoti ni tarehe …………..

1. MICHANGO YA SHULE

| S/N | AINA YA MICHANGO | KIASI |
|---|---|---|
| 1 | Mchango wa uendeshaji wa shule | 65,000/= |
| 2 | Tahadhari | 5000/= |
| 3 | Nembo | 5000/= |
| 4 | Kitambulisho | 5000/= |



KAGOMA HIGH SCHOOL (Education is the best opportunity)

| | | |
|---|---|---|
| | | |
| | JUMLA | 80,000/= |

NB: Fedha zote zilipwe kwenye akaunti ya shule
JINA: MDC KAGOMA SECONDARY
NAMBA YA ACCOUNT: 32001200063

2. MAHITAJI YA KUJA NAYO SHULENI

2.1. SARE YA SHULE

Unatakiwa kuwa na mavazi yafuatayo

i. Sketi mbili (KIJANI JESHI ILIYOKOLEA) Kitambaa Kizito (Esteem) yenye mshono wa malinda box, jumla ya malinda yawe kumi, mbele Matano na nyuma Matano (ziwe ndefu) iwe ma michirizi miwili ya kitambaa cha rangi ya blue bahari kwenye rinda la katikati. (Rangi hii ilikuwa changamoto kwa mwaka uliopita ikikuchanganya tuwasiliane kuepuka kununua sare mara mbili)
ii. Shati mbili mikono mirefu yenye rangi ya blue bahari (light blue) aina ya tetron(tomato) lenye vishikizo vya kawaida na mfuko mmoja upande wa kushoto (rangi hii ikikuchanganya mashati hayo unaweza kuyapata katika mazingira ya karibu na shule kwa gharama ya sh 15000)
iii. Soksi nyeupe jozi mbili (isiwe stoking)
iv. Tai moja ya kijani jeshi yenye michirizi ya blue bahari(tai zinapatikana kwenye mazingira ya shule kwa gharama ya TSH. 5000) kwa watakao hitaji kununulia hapa Shuleni
v. Sweta rangi ya ugoro yenye michirizi ya blue bahari shingoni na mikononi yenye nembo ya shule
vi. Viatu pea mbili rangi nyeusi visiwe na visigino virefu
vii. Tisheti moja rangi ya kijivu yenye kola ya mstari mweusi na kwenye mkono. Yenye nembo ya shule.
viii. Traka suti rangi ya light blue (isiwe ya kubana na isiwe ya kofia)
ix. Magauni mawili ya kushindia(shamba dress) rangi ya dark blue ( yawe marefu)
x. Viatu vya michezo raba nyeupe 1

KAGOMA HIGH SCHOOL (Education is the best opportunity)

xi. Kwa wanafunzi wa Kiislamu watatakiwa kuwa na sketi ya KIJANI JESHI ILIYOKOLEA (MBILI) zenye malinda boksi kumi Matano mbele na Matano nyuma, jarabibi ya rangi ya blue bahari mbili na Panjabi blue bahari mbili zenye urefu sawa na shati.

***NB: RANGI YA SARE IMEAMBATANISHWA HAPO CHINI***

2.2. Mwanafunzi anatakiwa kuja na vifaa vifuatavyo

i. Jembe moja na fyekeo moja
ii. Mifagio miwili (2) wa ndani 1 na wa nje 1, brashi kwa ajili ya usafi wa vyoo na bafu.
iii. Ndoo kubwa moja na ndoo ndogo moja Pamoja na beseni ya kuogea.
iv. Kifaa cha kutunzia maji ya kunywa
v. Vifaa vya usafi binafsi mfano mswaki, dawa ya meno kubwa, dawa ya viatu kubwa, mafuta ya kujipaka kopo kubwa, sabuni ya kufua na kuoga, kandambili/yebo na taulo
vi. Pair moja ya kitenge na vifaa kwa ajili ya usafi wa kimaumbile
vii. Ream 2 za karatasi kwa mwaka Aina ya double A( HATUPOKEI RIMU YA AINA NYINGINE TOFAUTI NA DOUBLE A)
viii. kokotoo (scientific calculator) la hesabu kwa wanaosoma sayansi
ix. mathematical set kwa wale wanaosoma Geography na sayansi
x. vitabu vya masomo ya Tahasusi yake
xi. Godoro lenye urefu wa futi 6 upana futi 2.5 (yanapatikana shuleni kwa gharama ya TSH. 47,000 kwa godoro la kawaida na kwa supa banko ni tsh70,000/=
xii. Taa ya betri/ solar kwa tahadhari ya umeme ukikatika (isiwe ya kuchaji kwenye umeme)
xiii. Faili mbili za Nailon (plastic file) la kutunzia mitihani,mazoezi na majaribio.
xiv. Vyombo vya chakula; Bakuli, sahani, Kikombe na Kijiko
xv. Nguo ya kulalia (night dress)
xvi. Taulo za kike zisizopungua paketi tano (5)
xvii. Nguo za ndani (gagulo underskirt), chupi za kutosha na sindiria 3 (nyeupe au nyeusi) toilet papers 5.
xviii. Kamusi ya Kiingereza kwa Kiingereza (advanced Dictionary) kwa wanafunzi wa masomo ya Sanaa

KAGOMA HIGH SCHOOL ( Education is the best opportunity)

xix. Mwanvuli mmoja
xx. Madaftari makubwa (counterbook) 7 three Quire/ four Quire na madaftari 5, two Quire kwa ajili ya mazoezi ya kila siku.
xxi. Kalamu za kutosha, Rula na penseli
xxii. Mashuka jozi mbili (2) rangi ya pinki, blanketi 1 nzito ( kuna baridi), mto mmoja na foronya 2 ( mashuka yawekewe alama ili kuepuka usumbufu wa kupotea). Pia aje na chandarua
xxiii. Bima ya afya (kama anayo)
xxiv. Tranka moja la bati na kufuli kwa ajili ya ulinzi.
xxv. Dissecting Kit ( kwa wanafunzi wa PCB)

NB: Hata hivyo Tai inaweza kupatikana mazingira ya karibu na shule kwa gharama ya shilingi 5000, Tshirt kwa gharama ya shilingi 16000 na sweta kwa gharama ya shilingi 20000.

3. MAMBO YA KUZINGATIA
   i. Hauruhusiwi kubadili Ngozi (kujichubua)
   ii. Rangi kwenye kucha, wanja,in ana urembo mwingine hauruhusiwi
   iii. Aje nan akala ya cheti cha uraia na nakala ya hati ya matokeo (result slip) ya kidato cha nne (muhimu)
4. SHERIA NA TARATIBU ZA SHULE ZINAZOPASWA KUFUATWA NA WANAFUNZI

Wakati wowote watu wanapoishi na kufanya kazi Pamoja huwa Hapana budi sheria na kanuni ziweke ili kurahisisha uhusiano mwema katika mwenendo wa wale wanaohusika. Sheria zifuatazo zimewekwa ili kusaidia mwanafunzi kujiepusha na mambo ambayo yanaweza kusababisha asihitimu masomo yake.

4.1. SHERIA NA KANUNI ZA SHULE KILA MWANAFUNZI ANAZOPASWA KUTII
   i. Heshima kwa viongozi,wazazi,wafanyakazi wote, wanafunzi na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.
   ii. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule ni muhimu
   iii. Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyingine zinazotolewa na viranja, walimu na walezi.

KAGOMA HIGH SCHOOL (Education is the best opportunity)

iv. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka ya shule wakati wote wa uanafunzi katika shule hii.
v. Kutunza usafi wa mwili na mazingira ya shule
vi. Kuvaa sare ya shule wakati wote inavyotakiwa
vii. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote

4.2. MAKOSA YANAYOWEZA KUSABABISHA MWANAFUNZI KUFUKUZWA SHULE

i. Wizi
ii. Uasherati na ushoga
iii. Ubakaji
iv. Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya kama vile uvutaji bangi,sigara,cocaine,mirungi, kuberi N.K
v. Kupigana au kumpiga mtu yeyote
vi. Kuharibu kwa makusudi mali ya umma
vii. Kudharau bendera ya Taifa
viii. Kuoa au kuolewa
ix. Kupata mimba au kuharibu mimba ndani na nje ya shule
x. Kutoa mimba
xi. Kugoma, kuchochea na kuongoza migomo au kuvuruga amani na usalama shuleni.
xii. Kukataa adhabu.
xiii. Mwanafunzi kuwa na simu ya mkononi

MUHIMU

- Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi
- Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye Bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumika kwa mwanafunzi mmoja.

KAGOMA HIGH SCHOOL ( Education is the best opportunity)

- ❖ Mwanafunzi ataruhusiwa Kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalumu toka kwa mkuu wa shule. (msiba au ugonjwa)

5. VIAMBATANISHO NA FOMU MUHIMU
   a) Fomu ya maelezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi na mkataba wa kutoshirki mgomo, fujo,na makosa ya jinai
   b) Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni, michango na maelekezo mengine yatakayotolewa na shule.
   c) Fomu ya uchunguzi wa afya (medical examination form) ambayo itajazwa na mganga mkuu wa Hospitali ya serikali (mwanafunzi atakayekuja bila kujaza fomu hii hatapokelewa)
   d) Picha nne za wazazi na ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi Pamoja na namba zao za simu. Mwanafunzi anaweza kutembelewa Jumapili ya mwisho wa mwezi tu kuanzia saa mbili asubuhi hadi saa kumi jioni.

Tafadhali soma kwa makini maelezo / maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

JE UNAKUBALI? NDIYO ………………… HAPANA…………………………

**NB: Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mitandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika kunahitajika pesa shuleni. TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/ MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE, NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBA ZIFUATAZO:**

**KWA MAWASILIANO ZAIDI TUMIA NAMBA HIZI**

**MKUU WA SHULE: 0762972449**

**MAKAMU MKUU WA SHULE (ADVANCE) 0777523527**

**MAKAMU MKUU WA SHULE: 0755220635**

**MWANDAMIZI TAALUMA: 0756856832**

……………………………………………………

MKUU WA SHULE

KAGOMA HIGH SCHOOL ( Education is the best opportunity)

SHULE YA SEKONDARI KAGOMA,
S. L. P 268,
MULEBA.
TAREHE: ……………………….

**KIAMBATANISHO A: MAELEZO BINAFSI YA MWANAFUNZI**

1. Jina Kamili la Mwanafunzi……………………………………………………………………………….
2. Anwani ya Nyumbani……………………………………………………………………………………
3. Mahali alipozaliwa:
   i. Wilaya………………………………………………………………………… ……………………
   ii. Tarafa ………………………………………………………………………………… ……………
   iii. Kata……………………………………………………………………………… ………………………
   iv. Kijiji/Mtaa……………………………………………………………………… ………………………
4. (a) Shule ya Sekondari ulipotoka……………………………………………………………………………….
   (b) Anwani ya Shule ulipotoka…………………………………………………………………………………
   (c) Mwaka aliomaliza Shule ya Sekondari………………………………………………………………….
   (d) Mchezo unaopendelea Zaidi……………………………………………………………………………….
5. Dini…………………………………………………………………………………………………… ……………………………
6. Wazazi (i) Jina la Baba……………………………………………………………..
   Anwani yake……………………………………………………………..
   Namba ya simu ya Mkononi…………………………………………
   Anaishi/amefariki(kata isiyohusika)
   Saini…………………………………………..

KAGOMA HIGH SCHOOL ( Education is the best opportunity)

(ii) Jina la Mama…………………………………………………………………

Anwani yake…………………………………………………………………

Namba ya simu ya Mkononi………………………………………………

Anaishi/amefariki(kata isiyohusika…………………………………

Saini…………………………………………………………………………………………………

(iii) Jina la mlezi (kama si baba au mama)

Anwani yake ……………………………………………………………

Namba ya simu ya mkononi……………………………

Uhusiano wake na wewe ni……………………………………………

Saini ya Mlezi……………………………………

(iv) Saini ya Mwanafunzi………………………

KAGOMA HIGH SCHOOL ( Education is the best opportunity)

**IJAZWE NA MZAZI/ MLEZI NA KURUDISHWA SHULENI**

ANWANI YA MZAZI/MLEZI
S. L.P ……………………….
………………………
TAREHE……………………

KUMB Na……………………….
MKUU WA SHULE
SHULE YA SEKONDARI KAGOMA,
S.L.P 268,
MULEBA.

YAH: MALEZI YA MTOTO………………………………………………KIDATO CHA………………………………………
TAHASUSI YA …………………………MWAKA ……………………………………………..

Nimezisoma sheria na Kanuni za shule Kumb. Na. KSS/ 02 na kuzielewa. Ninapenda kuhakiksha kwamba mimi mzazi/mlezi wa mtoto huyo/ niko tayari kusaidiana na shule katika jitihada zote za kumjengea mtoto wangu nidhamu ya dhati wakati wote awapo shuleni. Naahidi nitajitahidi kumwongoza kwenye masomo yake kulingana na taratibu za shule.

ZINGATIA

i. Asikose kuhudhuria shuleni kama hakuna sababu ya msingi ya kumzuia na akikosa, apewe kibali toka kwa mzazi/mlezi wake bila hivyo hatapokelewa.
ii. Asijihusishe na matendo ya utoro, uzururaji,matumizi ya madawa ya kulevya na vitendo vinginevyo ambavyo vinaweza kumzuia kuendelea na shule.
iii. Asipuuze au kukataa kuhudhuria miradi ya shule, kama vile kilimo na kutunza usafi wa mazingira.
iv. Asijihusishe na migomo au ushawishi wowote unaoweza kuvunja amani ya shule kwani kwa kufanya hivyo atafukuzwa shule mara moja.
v. Akazanie masomo kwa lengo la kufaulu mitihani yake ya ndani na ya nje.

KAGOMA HIGH SCHOOL ( Education is the best opportunity)

……………………………………………

………………………………

JINA KAMILI LA MZAZI/MLEZI
SAINI

KAGOMA HIGH SCHOOL ( Education is the best opportunity)

MEDICAL EXAMINATION FORM

DATE……………………………………………………………………………………

NAME OF STUDENT………………………………………………………………………………

To medical office I/C of ………………………………… District/ Regional/Referral/ Designated Hospital: P.O BOX ……………………………………………………….

Please examine the above named in full as to his/ her physical and mental fitness for Being able to pursue years of secondary school Education. In case of an acute Defect/disability in each category or subcategory may render the applicant ineligible of admission or eligible of admission to schools of students with special needs:

i. Blood pressure……………………………………………………………………………………………

ii. Sickle cell test……………………………………………………………………………………

iii. (a) eyesight………………………………………………………………………………………………

(b) Hearing……………………………………………………………………………………………

(c) Spleen……………………………………………………………………………………………

(d) Limps ……………………………………………………………………………………………………

(e) Venereal diseases………………………………………………………………………………………

KAGOMA HIGH SCHOOL ( Education is the best opportunity)

(f) Leprosy

…………………………………………………………………………………………………………
………..

(g) Epilepsy

…………………………………………………………………………………………………………
………

(h)
Typhoid……………………………………………………………………………………………
…………………….

iv. Neuroses

…………………………………………………………………………………………………………
………….

v. Other serious diseases

………………………………………………………………………………………………..

vi. Pregnancy

…………………………………………………………………………………………………………
………..

General comment(s)

…………………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………….

Name ………………………………………………
signature……………………..
Designation………………………………………………………………………………
…………………………..
Official
stamp………………………………………………………………………………………

Date……………………………………………….

KAGOMA HIGH SCHOOL ( Education is the best opportunity)

**ANGALIZO: Mzazi athibitishe kuwa vipimo hivi vimefanyika kikamilifu na siyo kujaz jina na sahihi ya mganga. Atakayegundulika shuleni kuwa hakuchukua vipimo kihalali atarudishwa nyumbani.**

**MKATABA WA KUTOSHIRIKI KATIKA MGOMO, FUJO NA MAKOSA YA JINAI**

Mimi …………………………………………………………………..nakiri kwamba sitoshiriki katika mgomo wowote, fujo yoyote, kuhudhuria Kikao kisicho na idhini ya utawala katika mazingira yote ya shule na kwamba sitoshiriki makosa yoyote ya jinai.

Nikiwa mwenye akili timamu naapa sitojihusisha na utovu wowote wa nidhamu na nitafuata taratibu/ sheria, ratiba kwa mujibu wa mipango ya shule. Na sitazungumza kauli yoyote ya kuchochea / kuhamasisha /kushinikiza / kushawishi uvurugaji wa amani ya shule/ mtu/kikundi/mdahalo. Sitashiriki majadiliano / maandamano/ mabishano yanayohatarisha amani ya shule.

Ikiwa nitatenda kinyume na niliyotaja hapo juu niwajibishwe kwa mujibu wa sheria za shule.

JINA LA KWANZA ……………… JINA LA KATI………………… JINA LA UKOO …………………..

SAINI: …………………………………. TAREHE: ……………………………

**UTHIBITISHO WA MZAZI/MLEZI**

Mimi………………………………………………………Mzazi/ mlezi wa ……………………………………… (mwanafunzi) nathibitisha kwamba mwanangu amesoma na kuelewa mkataba huu. Akienda kinyume na mkataba huu asimamishwe masomo mara moja na hatua za kinidhamu zichukuliwe dhidi yake.

SAINI………………………………Tarehe ……………………………… NAMBA ZA SIMU ………………………………………

KAGOMA HIGH SCHOOL ( Education is the best opportunity)



KAGOMA HIGH SCHOOL ( Education the best opportunity)





*Figure 1SCHOOL UNIFORM*

KAGOMA HIGH SCHOOL ( Education is the best opportunity)